GOVERNMENT NOTICE No. 105 published on 16/2/2024

SHERIA YA USIMAMIZI WA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128(2))*

AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA GARI MOJA LINALOINGIZWA NCHINI LA MRADI WA UJAZILIZI WA UMEME VIJIJINI MZUNGUKO WA PILI B WA WIZARA YA NISHATI, YA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Gari Moja Linaloingizwa Nchini la Mradi wa Ujazilizi wa Umeme Vijijini Mzunguko wa Pili B wa Wizara ya Nishati, ya Mwaka 2024, na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika kuanzia tarehe 15 Disemba, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuainishwa na Kamishna Mkuu, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na gari moja lililoainishwa kwenye Jedwali, linaloingizwa au kununuliwa ndani ya nchi na, au kwa niaba ya Wizara ya Nishati, kabla ya kugombolewa kupitia forodha kwa ajili ya kutumika mahususi katika utekelezaji wa Mradi wa Ujazilizi wa Umeme Vijijini Mzunguko wa Pili B, kimesamehewa.

Masharti

3. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba Amri hii haikutolewa, iwapo gari husika litatumika kwa madhumuni tofauti au litahamishwa, kuuzwa au kwa namna yoyote kupewa mtu mwingine asiyestahili kupata manufaa yanayotolewa chini ya Amri hii.

Ukomo

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 18 Juni, 2024.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Maelezo | Namba ya Chesesi | Namba ya Injini |
|---|---|---|---|
| 1 | Nissani Terra Station Wagon | MNTJCND23Z0006167 | YD25030137U |

Dodoma,
5 Februari, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*